Public Disclosure Authorized
Public Disclosure Authorized
Public Disclosure Authorized
Public Disclosure Authorized

WORLD BANK GROUP

MUHTASARI MKUU




# Kuelekea Uchumi JUMUISHI wa Zanzibar

## TATHMINI YA UMASKINI WA ZANZIBAR 2022

OCGS

# IKISIRI

Ripoti hii imetathmini maendeleo ya hivi karibuni ya kupunguza umaskini visiwani Zanzibar. Ripoti hii imetokana na matokeo ya tafiti tatu zilizopita za mapato na matumizi ya kaya (HBS) kwa kipindi cha kati ya mwaka 2009 na 2019, hasa kwa miaka minne ya mwisho ya muongo huo, yaani kati ya 2015 – 2019. Umaskini - kulingana na matumizi ya kwenye kaya - ulipungua kwa asilimia 9 kwa muongo uliopita kabla ya janga la UVIKO-19 ambapo ulipungua kutoka asilimia 34.9 hadi asilimia 25.7. Aidha, kasi ya kupungua kwa umasikini ilikuwa ndogo ukilinganisha na ongezeko la watu ambapo idadi ya watu maskini ilipungua kwa watu 27,000 tu. Umaskini ulipungua kwa haraka zaidi katika maeneo ya mijini. Matokeo ya uchambuzi wa hali tofauti za kitakwimu unaashiria kwamba umasikini wa mijini umeongezeka kwa asilimia 1.8 kwa kipindi cha kati ya 2020 – 21, wakati umaskini wa vijijini ulipungua kwa asilimia 0.8.

Mafanikio makubwa yalipatikana kwa kupitia viashiria visivyo vya kifedha. Katika kipindi cha 2009-2019, upatikanaji wa umeme uliongezeka kutoka asilimia 38 hadi asilimia 57, na viashiria vya elimu viliongezeka kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, kati ya mwaka 2015 na 2019, idadi ya wanafunzi walioandikishwa shule za sekondari (kidato cha I hadi IV) iliongezeka kutoka asilimia 68 hadi asilimia 90. Hata hivyo, kasi ya kupungua kwa umaskini ilikuwa ndogo ukilinganisha na ongezeko la idadi ya watu, kwani umaskini ulipungua kwa watu 27,000 pekee. Pengo la umaskini kati ya vijijini na mijini lilipanuka, kukiwa na tofauti kubwa kati ya visiwa vya Unguja na Pemba. Ukuaji wa uchumi kwa kipindi cha mwaka 2009 – 2019 haukuweza kusaidia kuboresha maisha ya watu waliokuwa katika umaskini uliokithiri. Ingawa katika kipindi cha kati ya mwaka 2014 hadi 2020 kulitokea mabadiliko makubwa kwa Zanzibar ambapo watu wengi waliacha kujishughulisha na kilimo kisicho na tija na kuhamia katika kazi za kutoa huduma, hasa wanawake (asilimia 10 walibadilisha shughuli za kiuchumi, kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa nguvukazi), ambapo uchambuzi wa kiuchumi unaonesha kuwa kitendo cha watu kubadilisha shughuli za kiuchumi kwa kuhamia katika sekta nyingine kumechangia kupunguza umaskini. Huenda walio wengi waliamua kuchagua kazi zenye tija ndogo za sekta ya huduma. Hakukuwa na uzalishaji wa kutosha wa ajira zenye staha, na ajira isiyo rasmi iliongezeka kwa kipindi husika. Aidha, matokeo ya kipimo cha umaskini cha MPI yaliyotokana na ukokotoaji wa vipengele vitatu na viashiria 13 vya utafiti wa Mapato na Matumizi Kaya (HBS) wa 2019-20 yalionesha kuwa asilimia 36.6 ya Wazanzibari walikuwa maskini kwenye vipengele vingi vya MPI, kwa maana ya kwamba walikuwa maskini kwa zaidi ya theluthi moja ya viashiria vilivyotumika vya MPI.

Ili kuharakisha kupunguza umaskini viziwani Zanzibar, inabidi kuufanya utalii, ambao ni injini kuu ya uchumi, kuwa jumuishi zaidi, kwa mfano, kwa kupanua zaidi huduma mbalimbali zinazohusiana na utalii. Pia ni vema kuboresha soko la ajira ili liweze kuwanufaisha wanawake na vijana kwa kuwapatia mafunzo ya ujuzi bora na programu za uanagenzi. Mwisho, ni kuboresha mazingira ya uendeshaji na usimamizi wa kampuni ndogo na za kati na kuwaunganisha wakulima wadogo na masoko yatakayowapa faida kubwa kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao, kutengeneza ajira na kupunguza umaskini.

Cover image by Agnieszka from Pixabay



Image by William Mgobela from Pixabay



Image by xiSerge from Pixabay

# MUHTASARI MKUU

*Umaskini ulipungua kabla ya janga la UVIKO-19, lakini kasi ilikuwa ndogo ukilinganisha na ongezeko la idadi ya watu, na pengo baina ya umaskini wa vijijini na mijini lilipanuka, likichochewa na tofauti kati ya visiwa vya Unguja na Pemba*


**Umaskini ulipungua kwa zaidi ya muongo mmoja kabla ya janga la UVIKO-19, lakini kasi ilikuwa ndogo ukilinganisha na ongezeko la idadi ya watu. Kiwango cha kupungua kwa umaskini** Zanzibar kilipungua kwa takribani asilimia moja kwa mwaka. Katika kipindi cha kati ya 2009 – 19, umaskini ulipungua kutoka asilimia 34.9 mnamo mwaka 2009 hadi asilimia 30.4 mwaka 2015, na asilimia 25.7 mnamo mwaka 2019, ikimaanisha kuwa umaskini ulipungua kwa asilimia 9.2 ndani ya kipindi cha miaka 10 (Kielelezo ES1a). Umaskini wa mijini ulipungua kwa haraka zaidi, ulikaribia kupungua kwa takribani nusu, wakati umaskini wa vijijini ulipungua kwa kiasi kidogo, kwa asilimia 15 tu. Kupungua huku kwa kiwango kikubwa kwa maeneo ya mijini, ambako viwango vya umaskini tayari vilikuwa chini, na kupungua taratibu katika maeneo ya vijijini, ambako tayari umaskini ulikuwa juu, kumesababisha kuongezeka kwa pengo la umaskini kati ya vijijini na mijini. Ilipofika mwaka 2019, umaskini wa vijijini ulikuwa mara mbili ya ule wa mijini. Hata hivyo, katika kipindi




Image by Jonas Thorén from Pixabay

cha mwaka 2015–19, umaskini wa vijijini ulipungua kwa haraka zaidi kuliko mijini, lakini kasi hii haikutosha kufidia pengo linalopanuka kati ya maeneo ya vijijini na mijini katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Zaidi ya hayo, idadi ya watu imekuwa ikiongezeka kwa takribani asilimia 2.8 kwa mwaka, ambapo ongezeko la watu linaendelea kuwa juu ukilinganisha na kiwango cha kupungua kwa umaskini. Matokeo yake ni kuwa idadi ya watu maskini ilipungua kwa kiasi kidogo sana, na katika maeneo ya vijijini idadi ya watu maskini iliongezeka kati ya mwaka 2009 na 2019 (Kielelezo ES1b).


**KIELELEZO ES1** **Matukio ya Umaskini na idadi ya watu maskini, ikioneshwa kwa maeneo katika mwaka 2009, 2015, na 2019**




*Chanzo:* tafiti za Mapato na Matumizi ya Kaya za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS) za mwaka 2009/10, 2014/15, na 2019/20. Ripoti ya utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya wa mwaka 2009/10 ilionesha umaskini ulipungua 209; kwa mwaka 2014/15 ulipungua mwaka 2015; na mwaka 2019/20 ulipungua 2019. Hivyo, tunarejea mwaka 2009, 2015 na 2019 kwa ajili ya kurahisisha ufafanuzi.

**Kuna tofauti kubwa ya umaskini katika mikoa, na tofauti za kimkoa zinazidi kupanuka**. Umaskini ulipungua kwa takribani nusu katika Mkoa wa Mjini Magharibi, lakini ulipungua kwa kiasi kidogo sana katika mkoani wa Kusini Pemba (Kielelezo ES2).

**KIELELEZO ES2** **Viwango vya idadi ya watu maskini (asilimia), ikiwa na asilimia 95 ya vipindi vya kujiamini. Ikionyeshwa kwa Mkoa, mwaka 2009 na 2019**




*Maelezo:* Mistari ya wima katika mche inaonyesha asilimia 95 ya vipindi vya kujiamini, ikimaanisha kuwa mabadiliko yana maana kubwa kitakwimu. Vipindi vya kujiamini ni vipana. Iwapo vitaingiliana kwa miaka miwili ya utafiti, basi tofauti haitokuwa na maana kitakwimu; hivi ndivyo ilivyo kwa mikoa yote, isipokuwa mmoja wa Mjini Magharibi. Kupungua kwa umaskini kwa Zanzibar yote kuna maana kubwa kitakwimu.
*Chanzo:* BOCGS HBS 2009/10 na 2019/20.



***Kukua kwa uchumi katika kipindi cha 2009–19 hakukuonekana katika kuimarika kwa ustawi wa maisha ya watu fukara, na “mnyumbuliko wa umaskini hadi ukuaji’ ulikuwa wa chini kama ilivyo kawaida kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.***

**Zanzibar ilishuhudia ukuaji mkubwa katika Pato Ghafi la Taifa (GDP) kwa mtu mmoja mmoja kati ya mwaka 2009 na 2019, lakini ukuaji huo haukuongeza matumizi kwenye kaya.** Ukuaji wa matumizi ya kaya katika kipindi cha mwaka 2009–15, na kipindi cha mwaka 2015–19 ulikuwa wa wastani na kwa kiasi kikubwa ulikuwa chini ukilinganisha na ukuaji wa uchumi uliotokea. Pato Halisi la Mtu Mmoja mmoja lilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 3 kwa mwaka, na kuongezeka kutoka Dola za Marekani 712 kwa mwaka 2009 hadi Dola za Marekani 950 kwa mwaka 2019, likiwa ni ongezeko la asilimia 33. Matumizi ya mtu mmoja mmoja, kadri ya matokeo ya tafiti za mapato na matumizi ya kaya (HBS), yaliongezeka kwa asilimia 18 tu kati ya mwaka 2009 na 2019. Kiasi kidogo zaidi ya nusu ya pato la mtu mmoja mmoja lilisababisha kuongezeka kwa matumizi ya kaya na kuboresha maisha ya watu, kwa mujibu wa utafiti wa mapato na matumizi ya kwenye kaya, ikiashiria kwamba ukuaji haukuwa mkubwa wa kuweza kuboresha maisha ya watu. Mnyumbuliko wa umaskini kuelekea ukuaji ulikuwa chini, na hili ni jambo la kawaida kwa nchi za Afrika Kusini mwa Sahara.



Image by Freija Carlsten from Pixabay

**Licha ya ukuaji wa kiasi wa Pato Ghafi la Taifa (GDP), utengenezaji wa ajira kwa kipindi cha 2014 na 2019-20 ulikuwa mdogo na ukosefu wa ajira uliongezeka kutoka asilimia 17 hadi asilimia 19, huku ukosefu wa kazi za kufanya pia uliongezeka kutoka asilimia 21 hadi 24. Hii ni kwa mujibu wa tafiti za nguvu kazi za mwaka 2014 na 2020–21.** Hali hii ilikuwa ngumu zaidi kwa wanawake ambao ukosefu wa ajira uliongezeka kwa upande wao kutoka asilimia 26 hadi asilimia 30, ambayo kwa sehemu fulani ilitokana na ukosefu wa ajira kwa vijana, hasa wasichana ambao ukosefu wa ajira kwa upande wao uliongezeka kutoka asilimia 41 hadi asilimia 48.[1] Hali ya kutokuwa na kazi za kufanya miongoni mwa wanawake iliongezeka kutoka asilimia 24 hadi 29. Watu wenye ajira zinazowapa ujira walikuwa asilimia 1.5 tu, ilikuwa juu zaidi ya mwaka 2019-20 kuliko mwaka 2014, na uwiano wa watu walioko kwenye sekta isiyo rasmi uliongezeka kwa asilimia 4 (asilimia 7 kwa wanawake). Matokeo ya utafiti uliofanywa kwa ajili ya kuutathmini MKUZA III yalionesha kuwa miongoni mwa washiriki waliohojiwa kuhusu maendeleo yaliyoonekana katika miaka 5 iliyopita, ni asilimia 0.3 walitaja shughuli za utalii. Ukosefu wa ajira ulitajwa na wengi kuwa ni miongoni mwa changamoto kubwa zaidi wanayokabiliana nayo.[2]

**Kaya zenye utajiri mkubwa zilinufaika zaidi kutokana na kukua kwa matumizi kati ya mwaka 2009 na 2019, na kwamba matokeo yake, kukosekana kwa usawa, ijapokuwa kwa kiwango kidogo, kuliongezeka kidogo sana miongoni mwa viashiria mbalimbali vya ukosefu wa usawa.** Makundi yote ya kaya yalipata ongezeko dogo katika matumizi halisi katika kipindi cha kati ya 2009 na 2019, lakini matumizi yaliongezeka zaidi kwa kaya tajiri kuliko kaya maskini. Watu fukara wapatao asilimia 40 walikuwa na ukuaji mdogo wa matumizi kuliko watu wote, na hivyo kufanya "**ushawishi wa ustawi wa pamoja**" kuwa hasi. Hii ilisababisha ongezeko dogo la ukosefu wa usawa, kama ilivyoakisiwa katika Kielekezi cha Gini kilichoongezeka kwa wastani tu kutoka 30.3 hadi 31.1. Kiwango hiki kiko chini zaidi kuliko ilivyo kwa Tanzania Bara (39.5 kwa mwaka 2018) na ni miongoni mwa vipimo vya chini zaidi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Ukosefu wa usawa uko juu zaidi katika maeneo ya mijini kuliko maeneo ya vijijini.

---

[1] Ajira kwa vijana wa kiume iliendelea kuwa ni asilimia 21

[1] SMZ (2017). Mkakati wa Kukuza Uchumi Zanzibar (MKUZA III), 2016 – 2020 Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

[3] Kutokana na data za utafiti wa Nguvu Kazi wa 2014 na 2020-21, lakini tafiti za mapato na matumizi ya kaya (HBS) za 2014/15 na 2019/20 zinaonesha mwelekeo unaofanana: idadi kubwa ya watu wanaofanya kazi kwenye kilimo, misitu na uvuvi ilipungua kwa asilimia 3.5, wakati idadi ya wanaofanya kazi kwenye sekta ya huduma iliongezeka kwa asilimia mbili. Hivyo sekta ya viwanda iliongezeka kwa asilimia 2.5

***Kuhama kwa watu wengi kutoka kilimo chenye tija ndogo kwenda kwenye huduma, hususani kwa Wanawake, kumechangia kidogo sana katika kupunguza umaskini. Kisiwani Unguja, sehemu kubwa ya watu maskini wako kwenye sekta ya huduma, ikiashiria kwamba hawakuweza kunufaika na sekta ya utalii inayokua kwa kasi.***

**Katika kipindi cha 2014 hadi 2020 - 21 watu wengi Zanzibar walihama kutoka kilimo chenye tija ndogo na kuingia katika sekta ya huduma[3], hususani wanawake (walihama kwa asilimia 10), lakini mchanganuo wa kina unaonesha kuwa kuhama kwa watu kwenda sekta nyingine za kazi kunachangia kidogo sana katika kupunguza umaskini.** Hii inaashiria kwamba kazi walizokuta katika sekta ya huduma hazikuwa na tija ya kutosha kuweza kuwainua kiuchumi na kuwa juu ya mstari wa umaskini. Ikiwa hili linatokea kipindi ambacho sekta ya utalii ilikuwa ikikua kwa kasi, basi hali hii inamaanisha kuwa mafanikio haya ya sekta ya utalii yamekuwa na mchango kidogo kwenye ustawi wa watu wa Zanzibar. Tafiti nyingine zinaonesha kuwa malipo mengi ya sekta ya utalii yanafanywa nje ya Zanzibar.




Image by Agnieszka from Pixabay

**Uwiano wa idadi ya watu wanaofanya kazi katika sekta ya huduma uliongezeka kwaharaka kutoka kwenye makundi ya watu fukara zaidi kuelekea kwenye makundi ya matajiri zaidi, lakini kwa upande wa kisiwa cha Unguja watu wengi kutoka kaya maskini wako katika sekta ya huduma** (angalia Kielelezo ES3). Hii inaashiria kwamba kufanya kazi kwenye sekta ya huduma hakuwafanyi waachane na umaskini. Kisiwani Pemba, takribani kila mtu aliye kwenye kundi la watu maskini anajishughulisha na kilimo. Kitendo cha watu kuhamia Mjini Magharibi iliyopo Unguja Magharibi kimetokana na kupungua kwa kiwango cha umaskini huko katika kipindi cha 2009–14, lakini umaskini haukupungua kwenye eneo hili katika kipindi cha 2015–19, hii inaashiria kwamba katika kipindi hiki kaya nyingi maskini zilizohamia Mjini Magharibi hazikuweza kupunguza umaskini.

**Sehemu kubwa ya wanawake maskini sana walioko Unguja ni wasichana waliokosa ajira au ambao hawana kazi za kufanya.** Kundi hili ni kubwa zaidi kuliko wanaume maskini. Ni dhahiri kuwa kitendo cha wanawake walioko Unguja kukosa kazi za kufanya, ingawa wana elimu ya kutosha, kimekuwa kikwazo kikuu cha kushindwa kupunguza umaskini. Wakati sekta ya utalii ikiwa ni kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi, inaonekana kuwa sekta hii imeshindwa kutoa ajira ya kutosha kwa idadi kubwa ya wanawake. Na hii huenda kwa kiasi fulani inatokana na wanawake wenyewe kutokuwa tayari kufanya kazi na wageni ambao wanadhani hawaendani na maadili na mila za kizanzibari. Lakini pia inaweza kuhusiana na ukosefu wa stadi zinazohitajika kwenye sekta binafsi na kushindwa kutengeneza ajira mpya.

**KIELELEZO ES3** **Sekta ya Kazi ya ajira kuu katika visiwa vya Unguja na Pemba, imefafanuliwa kulingana na ustawi wa kaya**




*Maelezo:* Umri wa wastani wa Wanawake kutoka kaya fukara kisiwani Unguja ambao hawana shughuli au wasiokuwa na ajira ni vijana zaidi kuliko watu waliobaki.
*Chanzo:* Tafiti za OCGS HBS 2019/20

## *Kuna idadi kubwa ya watu maskini kisiwani Pemba, ukichanganya na uduni wa huduma za jamii na fursa finyu za kiuchumi, hali inayoashiria kuwa watu maskini huko wameathiriwa na umaskini kieneo.*


Ukosefu wa usawa wa kieneo ni mkubwa na unaongezeka, kwani jitihada za kupunguza umaskini haziko sawa katika maeneo mbalimbali, wakati watu wengi maskini wakibaki katika lindi la umaskini wa kieneo (angalia Kielelezo ES4). Ingawa Pemba inachangia asilimia 27 tu ya watu wote wa visiwa vya Zanzibar, lakini zaidi ya nusu ya watu maskini (asilimia 57) wanaishi kisiwani Pemba. Hata kama kutafanyika jitihada za kuondoa tofauti za kielimu na sekta za ajira, kaya za kisiwa cha Pemba ziko chini ya kaya za Unguja kwa asilimia 6. Katika matumizi ya kawaida ya kila mtu mzima. Idadi kubwa ya watu wa kisiwani Pemba ni vijana, na ni asilimia 27 tu ya wakazi wake wako katika umri wa kufanya kazi (miaka 25 – 60) ukilinganisha na asilimia 36 za kisiwani Unguja, na matokeo yake ni kwamba viwango vya utegemezi viko juu zaidi kisiwani Pemba. Licha ya ongezeko la kasi, mafanikio katika sekta ya elimu yanaendelea kusuasua kisiwani Pemba, hususani kwa wanawake (angalia Jedwali ES1). Ijapokuwa upatikanaji wa umeme umeongezeka kwa kasi, uwiano wa idadi ya watu wanaopata umeme wa gridi bado ni nusu ya wale wa Unguja.

**Sura ya umaskini ya wananchi wanaoishi kisiwani Pemba ni tofauti sana na ile ya wale waliopo kisiwani Unguja**. Kisiwani Unguja, sehemu kubwa ya watu maskini hufanya kazi katika sekta ya huduma, wakati kisiwani Pemba takribani wote wako kwenye kilimo. Ni sehemu ndogo tu (asilimia 6 tu) ya malazi ya watalii yanapatikana Pemba. Ukosefu wa usawa wa kieneo unaoendelea kukua na kiwango kidogo cha huduma kwa maeneo ya watu maskini hususani yale ya kisiwani Pemba, miongoni mwa viashiria vingi vya kijamii, inaashiria kwamba watu maskini maeneo hayo wako katika lindi la umaskini wa kieneo.



Photo by Javi Lorbada on Unsplash

**KIELELEZO ES4** Mgawanyo kijiografia wa umaskini visiwani Zanzibar




*Chanzo:* OCGS HBS 2019/20.

**JEDWALI ES1** Wastani wa miaka ya kusoma (idadi ya watu wazima miaka 25-64)

| | 2015 | | | 2019 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| **Unguja** | 8.4 | 7.5 | 7.9 | 8.9 | 8.2 | 8.5 |
| **Pemba** | 6.1 | 4.6 | 5.3 | 6.7 | 5.2 | 5.9 |
| **Total** | 7.8 | 6.7 | 7.2 | 8.3 | 7.3 | 7.8 |


*Maelezo:* Hii inarejea kwenye idadi ya miaka shuleni iliyokamilishwa kwa mafanikio.
*Chanzo:* OCGS HBS 2019/20.

## *Zanzibar imepiga hatua kubwa katika utoaji wa huduma za kijamii, lakini bado kuna mapengo hususani katika wilaya maskini zaidi, hali inayosababishwa na matumizi ya serikali kwenye elimu na afya ambayo hayazingatii mahitaji ya maskini*

**Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita kumeshuhudiwa ongezeko kubwa upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii**. Upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii kuliongezeka kwa kasi katika wilaya zote. Hii imetokana na msukumo mkubwa wa uwekezaji katika utoaji wa huduma hizi katika kipindi cha miaka iliyopita ikiwa ni sehemu ya Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050.[4] Hii imewezesha kuboreshwa kwa viwango vya maisha na inawezekana kuwa imechangia sana katika kupunguza umaskini.

Mageuzi ya elimu ya hivi karibuni pamoja na kufuta ada za shule yamekuwa na matokeo ya kuvutia katika uandikishwaji wa wanafunzi. Kati ya mwaka 2015 na 2019, wastani wa viwango vya elimu kwa watu wenye umri wa kufanya kazi uliongezeka kwa asilimia 0.6 kwa watoto walioweza kumaliza shuleukilinganisha na wastani wa nchi nyingine za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Uandikishwaji uliongezeka kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, kuna tofauti kubwa kati ya makundi ya watu wenye uwezo na wasio na uwezo, na kuna tofauti kubwa ya kielimu kati ya maeneo ya vijijini na mijini, na kati ya visiwa vya Unguja na Pemba. Tofauti hizi za mafanikio kwa sehemu kubwa hazikurekebishwa katika kipindi cha kati ya mwaka 2014 na 2019. Kwa mwaka 2014, tofauti ya viwango vya uandikishwaji katika elimu ya msingi kati ya kaya fukara na tajiri sana ilikuwa asilimia 15, lakini iliongezeka hadi asilimia 22 ilipofika 2019. Kupanuka kwa pengo kunakofanana kumekuwa dhahiri zaidi katika ngazi ya elimu ya kati (angalia Kielelezo ES5). Viwango vya uandikishaji kwa elimu ya chini kwa wasichana viko juu kuliko wavulana.

**KIELELEZO ES5** **Viwango halisi vya uandikishaji kwa makundi tofauti ya utajiri, 2014 na 2019**




*Chanzo:* OCGS HBS 2014/15 na 2019/20.

[4] Soma http://planningznz.go.tz/doc/new/ZDV2050.pdf

**Viwango vya matumizi kwenye elimu kwa kila mwanafunzi vinatofautiana sana kwenye wilaya**. Matumizi ya serikali na ubora wa mazingira ya kujifunzia yako kiwango cha chini zaidi kwenye wilaya zenye viwango vya juu vya umaskini. Kwa mfano, katika wilaya ya Chake Chake kisiwani Pemba kuna wastani wa wanafunzi 92 kwa kila darasa la chekechea na msingi, ukilinganisha na wanafunzi 59 katika wilaya ya Kati, kisiwani Unguja. Mifumo ya kupanga shule na kupanga walimu ihakikishe kuwa walimu wapya wanapelekwa kwenye maeneo ya uhitaji na miundombinu inajengwa kuendana na mahitaji,. Hili likifanyika litaboresha mgawanyo wa fedha za umma.

**Viashiria vya afya viliboreshwa kwa kiwango kikubwa.** Kiwango cha wanawake kujifungua kwenye vituo vya afya uliongezeka kwa kasi kati ya mwaka 2010 na 2015–16, kulingana na Tafiti za Demografia na Afya (DHS) za kipindi cha miaka hiyo. Pia vifo vya watoto vilipungua sana na viko chini ya vile vya Tanzania bara. Ongezeko la wanawake wajawazito kujifungulia kwenye vituo vya afya pamoja na watoto wengi kupata chanjo yamekuwa ni mambo muhimu yaliyochangia kupungua kwa vifo vya watoto.



Image by Hans from Pixabay


Photo by Anil Reddy on Unsplash

**Watu maskini wanaugua mara nyingi zaidi, lakini huenda kufuata huduma rasmi za afya mara chache zaidi ya matajiri.** Hivyo, matumizi kwenye huduma ya afya hayalengi zaidi watu maskini. Takwimu zinazohusu gharama za afya za serijali kwa kichwa kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ikijumuisha na taarifa za utafiti wa mapato na matumizi ya kaya (HBS) zinaonesha kuwa Serikali inatumia fedha nyingi zaidi kwenye sekta ya afya inayowanufaisha zaidi matajiri kuliko watu maskini.

**Kaya nyingi za Zanzibar (asilimia 91) zinapata maji salama ya kunywa lakini uboreshaji wa uwiano wa kaya zinazopata huduma ya maji ya bomba (mfereji) umekuwa kasi ndogo: uliongezeka kutoka asilimia 32 mwaka 2009 hadi asilimia 36 mwaka 2019.** Kaya zinazopata maji ya bomba ndani au nje ya makazi ziliongezekea kutoka asilimia 80 mwaka 2009 hadi asilimia 82 mwaka 2019, lakini ongezeko katika kipindi hiki cha miaka kumi lilikuwa dogo sana katika maeneo ya vijijini kwa asilimia 1 tu, ikilinganishwa na asilimia 4 kwa maeneo ya mijini. Upatikanaji wa huduma za vyoo uliongezeka kwa kiasi kikubwa katika muongo uliopita, kwani idadi ya kaya zilizo na vyoo vya kisasa na mfumo wa kusafisha maji iliongezeka kutoka asilimia 20 hadi 51 kati ya 2009 na 2009.

**Upatikanaji wa umeme uliongezeka kwa kiwango kikubwa katika muongo mmoja uliopita.** Idadi ya kaya zinazopata umeme kutoka gridi ya taifa iliongezeka kutoka asilimia 38 hadi 57 kati ya 2009 na 2019. Wakati asilimia 6 nyingine wakipata umeme wa jua (kwa sehemu kubwa maeneo ya vijijini). Sehemu ya wanaotegemea vibatari vya mafuta ya taa ilipungua kwa nusu. Kuhakikisha




kwamba watu maskini wanapata huduma za kisasa za nishati, ni moja ya vipaumbele vya kimkakati kwa sekta ya nishati Zanzibar, ambayo imefafanuliwa kwa kina katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA III).

**Kiwango cha Umaskini wa Kukosa Kipato na Huduma visiwani Zanzibar, kwa kutumia kipimo cha MPI kilikadiriwa kuwa asilimia 36.6 mwaka 2019.** Kiwango cha umaskini wa kukosa kipato na huduma kinatambuliwa endapo mtu anakosa walau theluthi moja ya viashiria 13. Miongoni mwa watu ambao ni maskini wa kipato na huduma asilimia 16 wanaishi maeneo ya mijini, wakati asilimia 84 wanaishi maeneo ya vijijini. Zaidi ya nusu ya Wazanzibari wanaoishi maeneo ya vijijini wana umaskini wa kukosa kipato na huduma, wakati kwenye maeneo ya mijini asilimia 14 tu.

**Kama ilivyo kwa umaskini wa fedha, Kaskazini Pemba ina idadi kubwa (asilimia 72) ya watu walio na umaskini wa kukosa kipato na huduma**, wakati Mjini Magharibi, eneo lenye watu wengi zaidi, lina kiwango cha chini zaidi cha umaskini wa kukosa kipato na huduma (asilimia 14). Umbali wa kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za kijamii inaonesha uhusiano ulipo kati ya MPI katika ngazi ya wilaya. Chini ya nusu ya watu walio na umaskini wa kukosa kipato na huduma, pia walikuwa maskini wa kifedha, na hii inaonesha umuhimu wa kutumia vipimo vyote vya umaskini kwa ajili ya kufuatilia ukuaji maendeleo na kutunga sera na kuandaa mipango.

***Wepesi wa kuathirika na mishtuko uko juu kadri kaya nyingi zinavyoingia na kutoka kwenye umaskini; hata hivyo, wachache wanaweza kupata huduma za mpango wa kunusuru kaya maskini kwa mujibu wa data za utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS), na kwa kiasi kikubwa mitikisiko ya kiuchumi huathiri kasi ya kupunguza umaskini; kuna nafasi ya kuboresha utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ili matokeo yake yasaidie kufuatilia vizuri zaidi programu zinazowalenga watu maskini.***

**Wepesi wa kuathirika kiuchumi uko juu.** Sehemu kubwa ya watu wa Zanzibar wako karibu na mstari wa umaskini hivyo inakuwa kirahisi kwao kuangukia kwenye umaskini. Na sehemu kubwa ya watu wa Zanzibar huingia na kutoka kwenye umaskini: kati ya mwaka 2008–09 na 2012–13, asilimia 22 ya watu wa Zanzibar walikuwa kwenye "umaskini wa muda kidogo" au "umaskini wa msimu," kutokana na matokeo ya ufuatiliaji wa kaya (NPS) wa mwaka 2008–09, 2010–12, na 2012–13.

**Janga la UVIKO-19 linaelezwa kuwa limechangia kuongeza umaskini kutokana na kaya nyingi kupata mtikisiko wa kiuchumi na kukosa uwezo wa kukabiliana nao.** Visiwani Zanzibar, athari za janga la UVIKO-19 zilionekana katika sekta ya utalii ambapo watalii walipungua na ukosefu wa ajira na kuyumba kwa shughuli za biashara vilisababisha kuongezeka kwa umaskini mijini kwa asilimia 1.8 ndani ya kipindi cha 2020–21. Kwa mujibu wa utafiti wa kitaifa



Image by Agnieszka from Pixabay

kwa kutumia simu,[5] asilimia 6 ya waliohojiwa waliokuwa wakifanya kazi kabla ya janga mnamo Januari 2020, walieleza kuwa hawakuweza kuendelea kufanya kazi kwa kipindi kilichosalia cha mwaka. Idadi kubwa ya walioathiriwa zaidi walikuwa wanawake ambao walikuwaasilimia 33 dhidi ya asilimia 12 za wanaume.

**Fedha zinazotengwa kwa ajili ya hifadhi ya jamii zimeongezeka kwa miaka ya hivi karibuni, lakini utafiti wa mapato na matumizi ya kaya (HBS) haiwezi kufanya tathmini ya kutosha kuhusu utoshelevu wa mifuko ya pensheni na uhifadhi ya jamii na mpango wa uhawilishaji wa fedha wa TASAF.** Fedha nyingi zinazotumika katika hifadhi ya jamii kwa sehemu kubwa zinatokana na bima za kijamii. Data zilizotokana na tafiti za mapato na matumizi ya kaya (HBS) pamoja na ufuatiliaji wa kaya (NPS) zinaonyesha kwamba bado programu za msaada wa kijamii hazijawafikia wengi ingawa bado kuna uwezekano wa kuboresha ili kuwafikia watu maskini. Wakati misaada inayotolewa na TASAF inalenga kuwanufaisha zaidi maskini wa kipato, programu nyingine za msaada wa kijamii zimeonesha kupwaya kwa kujielekeza zaidi kwa watu wenye uwezo. Hata hivyo, kuna sababu ya kuamini kuwa tafiti za mapato na matumizi ya kaya hazijaweza kubainisha vya kutosha kiwango cha ufikiwaji wa huduma za hifadhi ya jamii. Kuna uwanda wa kuboresha ubunifu zaidi wa utafiti na utekelezaji kuhusu kurekodi data kutoka kaya, kwa ajili ya Programu za sasa ambazo zimewekwa kwa ajili ya kusaidia watu maskini.



Photo by Kaspars Eglitis on Unsplash


[5] Ripoti za ufuatiliaji kuhusu hali ya maisha ya watu nchini Tanzania: soma kupitia https://www.nbs.go.tz/index.php/en/censussurveys/poverty-indicators-statistics/national-panel-survey/743-tanzania-high-frequency-welfare-monitoring-survey

## *Licha ya kuwepo kwa tofauti ndogo ya kijinsia kwenye mafanikio ya elimu, matokeo ya soko la ajira yanatofautiana pakubwa kati ya wanaume na wanawake; sehemu kubwa ya muda wao unatumika kwenye kazi za nyumbani zisizo na ujira na kazi za malezi*

**Ijapokuwa mafanikio ya kielimu kwa wanawake yanakaribia yale ya wanaume, bado kwenye ajira wameachwa nyuma zaidi.** Ingawa wanawake wako nyuma ya wanaume kielimu kwa tofauti ya mwaka mmoja, lakini kwa mwaka 2020–21 ni asilimia 50 tu ya wanawake walikuwa wakifanya kazi za ujira au walijiajiri, ukilinganisha na asilimia 73 ya wanaume. Inaonekana wanawake hawajatumika kiasi cha kutosha kama rasilimali watu muhimu, na kuacha uwezo wao wa kuinua vipato vya kaya kutokutumika ipasavyo. Kiwango cha ajira kwa wanawake kiko chini sana kuliko ilivyo kwa Tanzania nzima licha ya viwango vyao vya juu zaidi vya elimu (Kielelezo ES6). Miongoni mwa wanawake wanaofanya kazi, wao wanaofanya kazi za ujira ni wachache kuliko wanaume, asilimia 33 dhidi ya asilimia 21—na pengo hilo limekuwa likipungua taratibu mno.


Tofauti ya muda unaotumika katika kazi za kulipwa na kutokulipwa unatofautiana sana kati ya wanaume na wanawake. Kwa wastani wanaume hutumia chini ya masaa matatu ya kazi za kulipwa kuliko ilivyo kwa wanawake wanaofanya kazi za kulipwa. Kwa upande mwingine, wanawake hutumia zaidi ya mara sita ya saa wanazotumia wanaume wanaofanya kazi za nyumbani zisizo za malipo, wakati kwa ujumla wanaume hutumia muda mchache sana wa kufanya kazi za nyumbani zisizo za malipo. Pengo la kijinsia katika kazi zisizo za malipo ni kubwa zaidi kwenye maeneo ya mijini kuliko maeneo ya vijijini (angalia Kielelezo ES7) lakini hakuna pengo la kijinsia kwa makundi ya watu wenye uwezo (ikifafanuliwa kwa viwango vya matumizi), wakati muda wa wanawake uliotumika kwenye kazi za malipo (kwa maana ya kazi zinazotambuliwa kwenye Mfumo wa Hesabu za Taifa (SNA) huongezeka kwa wastani kwa makundi ya kaya yanayopokea huduma za hifadhi ya jamii.

**KIELELEZO ES6** **Ajira miongoni mwa wanaume na Wanawake, mwaka 2014 na 2020/21**




*Maelezo:* Ajira inafafanuliwa kuwa ni kufanya kazi kwa malipo na inajumuisha kujiajiri,
*Chanzo:* Kutokana na Tafiti Jumuishi za Nguvu Kazi (ILFS) 2020-21

**KIELELEZO ES7** **Muda wa wastani unaotumiwa na wanaume na wanawake wenye umri wa miaka 15 na zaidi kwa siku kwenye majukumu kwa eneo (saa kwa siku yenye saa 24)**




*Maelezo:* 'Kazi za malipo' inamaanisha kazi zile zinazochangia kwenye Mfumo wa Hesabu za Taifa (SNA), wakati kazi zisizo za malipo kama kazi isiyoingia kwenye Mfumo wa Hesabu za Taifa (SNA), kama vile kazi za nyumbani zisizo na ujira, na matunzo.
*Chanzo:* OCGS HBS 2019-20



Photo by Kaspars Eglitis on Unsplash

## Kuharakisha kupunguza umaskini, hatua kadhaa za kisera zizingatiwe:

### Kuufanya utalii kuwa jumuishi zaidi na kukuza fursa za kiuchumi kisiwani Pemba

**Kutumia vizuri fursa zinazotokana na sera ya Zanzibar ya "uchumi wa bluu" kwa ajili ya kutanua huduma za utalii ili uweze kuwanufaisha watu wengi zaidi.** Kwa jili ya kuwanufaisha zaidi wananchi kiuchumi na kijamii, mambo yafuatayo ni muhimu:

- Kuhimiza uanzishwaji wa hoteli ndogo ndogo zinazomilikiwa na wenyeji zitakazotoa huduma za malazi kwa watalii. Programu ya kuwa na mfumo wa kutanganza ubora wa huduma za ndani, itakayofanana na programu ya Visiwa vya Shelisheli (Seychelles Secrets); na Programu kama hiyo ya visiwa vya Cabo Verde, inaweza kutayarishwa ili kutoa mafunzo, ithibati, na kuhamasisha uanzishwaji wa hoteli ndogo ndogo zinazomilikiwa na wenyeji zinazotoa huduma za malazi katika visiwa vya Pemba na Unguja.
- Kuweka miundombinu na kuvutia uwekezaji kisiwani Pemba (kwa sasa ni asilimia 5 tu ya vitanda iko katika kisiwa hiki).
- Kuanzisha vikundi vidogo vitakavyosambaa maeneo ya vijijini na kuwa na shughuli mbalimbali, na ikiwezekana shughuli hizo zisimamiwe na wanajamii wenyewe. Vikundi hivyo vipewe nafasi ya kuwekeza kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Msitu wa Jozani, utalii wa kilimo, na utalii wa bahari.

Juhudi kubwa zaidi zinahitajika ili kupunguza uharibifu wa mazingira, upotevu wa bioanuwai, na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za bahari.



Photo by Mathias Katz on Unsplash

**Ipo haja ya kuimarisha zaidi muunganiko kati ya sekta ya utalii na uchumi wa ndani kwani zaidi ya asilimia 80 ya mahitaji katika sekta ya utalii huletwa kutoka nje ya Zanzibar**. Hali hii inasababishwa na ukweli kuwa ubora na wingi wa bidhaa na huduma za ndani ya Zanzibar haviendani na matakwa ya viwango vya bidhaa na huduma zinavyohitajika katika sekta ya utalii . Ili kuhakikisha kuwa chakula kinachozalishwa kinakidhi mahitaji ya chakula kwenye hoteli za kitalii kwa mwaka mzima, basi ni vema kujielekeza katika kuwanganisha wakulima wadogo wadogo wajiunge na kilimo cha mkataba. Unaweza kuanzishwa mtandao wa vituo vya ukusanyaji, kutibu, na usambazaji vitakavyosimamiwa na sekta binafsi ambao utawajibika katika kutoa mafunzo kwa wakulima na wahusika wengine wa mnyororo wa thamani, na kukusanya na kusambaza taarifa za masoko. Pia kuna uwezekano wa kupunguza gharama za uendeshaji kwa kupitia suluhisho za kidigitali, kama vile kutengeneza programu tumizi zitakazorahisisha shughuli za upatikanaji wa leseni na usajili, kuweka kumbukumbu, na malipo kwa njia ya mtandao.

### *Kuboresha soko la ajira ili lilete matokeo bora kwa wanawake na vijana*

**Ili vijana na wanawake waweze kunufaika na soko la ajira inabidi kujielekeza zaidi katika kuboresha mafunzo ya ujuzi na kuwa na programu za uanagenzi ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kutumia ujuzi wao wa kiufundi na stadi za maisha.** Uimarishaji wa ujuzi unahitajika hususani katika kuboresha huduma kwa wateja na stadi za maisha zinazohitajika katika sekta ya hoteli. Ili kuwawezesha wanawake waweze kutumia vyema fursa za kiuchumi zilizopo inabidi


Photo by Olga Budko on Unsplash




kufanyike mageuzi katika masuala ya kijinsia na mitazamo ya kidesturi kuhusiana na kazi za nyumbani zisizo na ujira, pia ni muhimu kuwepo na vituo vya kutunza watoto.

### *Kuifanya elimu iwanufaishe watu maskini kwa kuiboresha elimu inayotolewa kwenye taasisi za umma*

**Ili kupunguza mapengo ya utoaji wa huduma kwenye shule inabidi kufanya maboresha ya mfumo wa upangaji wa shule na vituo vya kazi kwva walimu kwa kuhakikisha kuwa walimu wapya wanapelekwa kwenye shule zinazohitaji walimu zaidi na pia miundombinu ya shule ijengwe kwa kuzingatia mahitaji.** Fedha zaidi zinapaswa kutengwa kwa ajili ya kuongeza wigo wa elimu kwa watoto ambao kwa sasa hawapati nafasi ya kwenda shule. Utaratibu huu unahusu kuanzishwa kwa shule zaidi za serikali za sekondari, na kuhakikisha walimu wanapatikana pamoja na vifaa vya kujifunzia. Pili, juhudi kubwa zaidi zinahitajika katika kuwafikia watoto walio pembezoni zaidi ili waweze kuandikishwa na kuanza masomo na wasaidiwe waendelee na masomo hadi wanafika mwisho.

### *Matumizi ya umma yawajali zaidi watu maskini*

**Msingi wa kupambana na umaskini ni kujenga uhimilivu wakati wa mtikisiko wa kiuchumi.** Kuwa na uhimilivu maana yake ni kuwawezesha watu "kurejea kwenye hali zao za awali baada ya mtikisiko" wakati dunia inakabiliwa na majanga mbalimbali. Ili kuwa na uhimilivu inatakiwa pawepo na na akiba ya kutosha ya fedha, mtaji wa mali isiyohamishika, na kuboresha upatikanaji wa huduma za hifadhi ya jamii na bima ya afya. Upatikanaji na ufanisi wa utaratibu wa uhawilishaji wa fedha na bima ya afya vinaweza kufuatiliwa vizuri zaidi kupitia mifumo ya usimamizi wa taarifa, ikiwemo tafiti za mapato na matumizi ya kaya (HBS). Kaya zenye watoto wadogo zisaidiwe kwa kupitia mfumo wa kusaidia kaya maskini kwa njia ya uhawilishaji wa fedha ili ziwezeshe kaya hizo kupata chakula cha kutosha. Mpango huu unaweza kufanyika kwa njia ya ruzuku ya mtoto itakayotolewa kupitia mama hadi mtoto anapofikisha miaka miwili. Ili kuwezesha upatikanaji mzuri wa huduma za afya kwa watu maskini, ni vema kuhakikisha kuwa ubora wa huduma na msamaha wa malipo unahusisha pia vituo binafsi vya kutolea huduma za afya.

### *Kuboresha mazingira ya uendeshaji na usimamizi wa kampuni ndogo na za kati kwa ajili ya kuongeza thamani mazao ya ndani na kutengeneza ajira zaidi.*

Kuna fursa za kuimarisha mazingira ya biashara kwa ajili ya kampuni ndogo na za kati zinazojihusisha na kukusanya na kuchakata mazao ya ndani kama vile mwani na chumvi ambazo zinaweza kuwa chanzo muhimu cha mapato kwa wanawake maskini. Uwezekezaji katika umwagiliaji na huduma za kukusanya mazao unaweza kuwa wa manufaa endapo uzalishaji wenye tija katika kilimo utaendelezwa na hivyo kuwa na uhakika wa kusambaza mazao ya chakula kwenye mahoteli kwa mwaka mzima. Huduma bora za fedha kwa wale wanaoanza biashara na kulinda haki miliki, stadi za biashara, kujitangaza, viwango bora vitahamasisha ubunifu na utengenezaji ajira. Kuimarisha majadiliano kati ya sekta binafsi na ya umma ni jambo muhimu kwa ajili ya kufikia mageuzi yanayohitajika.




Photo by Raissa Lara Lutolf Fasel on Unsplash

WORLD BANK GROUP